Australian Government

Tuition Protection Service

# Mchakato wa Usaidizi kwa Wanafunzi unaofuata Kushindwa kutekeleza kwa Mtoa Elimu

Mtoa wako wa elimu au mafunzo:

- anafunga, anashindwa kuanza kozi uliyojiandikisha, au anaacha kutoa kozi yako kwa sehemu ya muda; na
- mtoa masomo hana uwezo wa kukurejeshea ada yako ya masomo, harudishii ada zako za masomo, au hakupanga ukamilishe masomo yako na mtoa masomo mwingine.

TPS inaita hii **kushindwa kutekeleza kwa mtoa'**.

**TPS** inawasiliana nawe kwa kutumia maelezo ya mawasiliano uliyompa mtoa wako.

**TPS** inakualika kuhudhuria kipindi cha taarifa ili kutoa ushauri kuhusu kufanya nini baadaye na kukuonyesha jinsi ya kutumia mfumo wa usimamizi wa kesi wa TPS Online.

**TPS** inakutumia barua pepe ya kuingia. **Wewe** unaweza kupata TPS Online kupitia kwa www.tps.gov.au.

**Wewe** unaingia kwa TPS Online.

Kwenye TPS Online, **wewe** utahitaji kubadilisha neno lako la siri, kueleza kama mtoa wako alitimiza wajibu wake kwako, kupakia kitambulisho cha picha (pasi au leseni ya dereva), na kusasisha maelezo yako ya mawasiliano.

**TPS** inaweza kukusaidia kupata chaguzi zinazofaa za kuanza/kuendeleza elimu yako na mafunzo na mtoaji mbadala wa Australia.

Kama mtoa mbadala mwingine hapatikani, au muda wa uhamisho wa kozi umeisha, **TPS** itatathmini dai lako la kurejeshewa ada yoyote uliyolipa ambayo tayari haijatumiwa na mtoa huduma wako katika kutoa elimu yako na mafunzo.

TPS inaita hii **'ada za masomo ambazo hazijatumika'**.

**Wewe** utahitaji kutoa TPS na hati za kifedha zinazoonyesha ada zako za kozi na ushahidi wa malipo yote yaliyofanywa kwa mtoa huduma wako (na wakala wako, kama unaye mmoja). Hati hizi ni lazima ili kuhesabu marejesho yako.

**TPS** inahesabu kiasi chako cha kurejesha na kukutumia barua pepe ili kutoa maelezo ya akaunti ya benki kwenye TPS Online.

**Wewe** hutoa maelezo ya akaunti ya benki kwenye TPS Online. **TPS** hurejesha malipo yako ya ada ya masomo ambayo hujatumia kwenye akaunti yako ya benki uliyochagua.



Ikiwa wewe na mwanafunzi wa kimataifa, **wewe** utahitaji kujiandikisha na mtoa mwingine katika miezi mitatu ili kuendelea kusoma nchini Australia na kutimiza mahitaji ya visa yako ya mwanafunzi.

**Wewe** unaendelea kusoma nchini Australia.

**Tovuti:** www.tps.gov.au **| Barua Pepe:** support@tps.gov.au **| Simu:** 1300 131 798